# AFYA YA AKILI YA WAHAMIAJI

*Katika Carolina Kasazini*



**Taasisi ya Tiba ya Carolina Kaskazini** na **El Futuro** ilikusanya taarifa ili kuelewa vizuri nguvu na changamoto ambazo wahamiaji katika NC wanakabiliana nazo kuhusu afya yao ya akili. Hapa kuna baadhi ya vizuizi vilivyopatikana na baadhi ya suluhisho ambazo viongozi wa jamii wanaweza kutekeleza.

## KUANZIA VIZUIZI HADI VITENDO

### UNYANYAPAA

**Hofu** ya **kuhukumiwa** au kutengwa kunaweza kusababisha wengine **kutotaka kujihusisha na huduma za afya ya akili**

### FANYA IWE KAWAIDA

- Kuwa na mazungumzo ya mara kwa mara kuhusu **afya ya akili** katika jamii yako
- Kukuza eulewa wa afya ya akili **na upatikanaji wa rasilimali** miongoni mwa viongozi wa jamii
- Weka semina za **afya ya akili** katika **makanisa** au makundi **mengine**

### UFIKIAJI WA LUGHA

Uhaba wa watoa huduma **wanaozungumza lugha ya asili** ya wahamiaji unaweza **kusababisha** huduma **ya kiwangocha chini**

### VUNJA VIZUIZI

- Kuongeza **uwekezaji** kwa wafanyikazi wanaozungumza lugha mbili ili kuwasaidia wahamiaji kuelewa au kutumia mifumo iliyopo
- Tengeneza **mwongozo** wa watoa huduma wanaozugumza lugha mbili na rasilimali katika eneo lako
- **Wasaidie** majirani wahamiaji kuwa wataalamu wa afya ya akili wanaozungumza lugha **mbili**

### UKOSEFU WA BIMA

Wahamiaji wengi **hawafuzu** kupata bima za afya za serikali na **hawawezi kupata bima zinazotolewa na waajiri**

### UNGANISHA NA RASILIMALI

- **Unganisha** jamii isiyo na bima na **huduma za bure** au **za gharama** nafuu
- Andaa **matamasha ya afya ya kijamii** ili kuunganisha jamii yako na watoa huduma
- Wasaidie wengine **kujaza fomu na makaratasi** ili wafuzu kupata **huduma zilizopunguziwa bei**

***Je, ungetaka kujua zaidi?*** *Changanua msimbo huu wa QR ili kupata uchambuzi kamili wa mazingira haya.*

# AFYA YA AKILI YA WAHAMIAJI

*Katika Carolina Kasazini*



# MAELEZO YA JUMLA KUHUSU WAHAMIAJI WA NORTH CAROLINA

*Imeandaliwa kwa ajili ya viongozi wa jamii na mashirika yaliyojitolea kuboresha afya ya akili ya wahamiaji.*

## *Ni nani wahamiaji wanaoishi Carolina Kaskazini?*

**8%**

Asilimia ya idadi ya watu wa NC ambao ni wahamiaji waliozaliwa nje ya nchi

**Mtoto 1 kati ya 5** huko NC ana mzazi angalau mmoja 1 ambaye ni mhamiaji

**Amerika ya Kilatini: ~520,000**
**Asia: ~264,000**
**Ulaya: ~104,000**
**Afrika: ~85,000**
**Australia na Pasifika: ~2,500**

## *Wahamiaji wanachangiaje katika kuimarisha Carolina Kaskazini?*

**$9.8 BILLIONI**

Jumla ya michango ya kodi kutoka kwa wahamiaji katika North Carolina

**BIASHARA**

38% ya kampuni za Fortune 500 zilizopo NC zilianzishwa na wahamiaji wa kizazi cha kwanza/pili

**602,600**

Jumla ya wafayikazi wahamiaji katika NC

### *Mtazamo wa vipaumbele*

Kwa watu wengi, afya ya akili inaweza kupewa kipaumbele cha chini ikilinganishwa na afya ya kimwili na mahitaji mengine muhimu. Maisha ya kiuchumi yanaweza kutawala fikra za wahamiaji wengine, kwani kupata kazi thabiti, makazi, na chakula ni mambo muhimu kwa ustawi wa familia.

> ***"Kuna unyanyapaa mwingi, na hofu nyingi. Wateja wangu wengi huniambia, 'unajua, sitaki familia yangu ijue kuwa niko hapa nikizungumza nawe.'"***
>
> -Nukuu kutoka kwa mtaalamu wa afya anayehudumia wahamiaji

### *Kwa nini kuna takwimu chache sana kuhusu jamii za wahamiaji?*

Katika jamii nyingi za wahamiaji, kuna unyanyapaa mkubwa wa kitamaduni unaohusishwa na ugonjwa wa akili, hali inayowafanya watu kuepuka kujadili maswala haya waziwazi au kutafuta msaada wa kitaalamu kwa hofu ya kutengwa na jamii.

**LUGHA 20 BORA ZENYE IDADI KUBWA YA WASEMAJI AMBAO PIA WANAZUNGUMZA KIINGEREZA CHINI YA KIWANGO CHA CHINI YA "VIZURI SANA" (IDADI YA WASEMAJI, 2022)**

| | |
|---|---|
| Kihispania | Wazungumzaji 330,018 |
| Kichina (Kimandarini, Kikantoni) | 17,062 |
| Kivietinamu | 13,592 |
| Kiarabu | 10,910 |
| Kikorea | 8,208 |
| Kigujarati | 6,845 |
| Kifaransa | 6,425 |
| Kirusi | 5,397 |
| Kitelugu | 4,860 |
| Kiingereza, Kisamoa, Kihawaii, au Lugha nyingine za Austronesia | 4,748 |
| Kithai | 4,288 |
| Kiamhari | 4,121 |
| Kihindi | 4,062 |
| Kihmong | 3,912 |
| Kireno | 3,885 |
| Kijapani | 3,566 |
| Kijerumani | 3,400 |
| Kitagalog | 3,349 |
| Kinepali | 3,104 |
| Kikrioli cha Haiti | 3,012 |

Ikiwa ungependa kujifunza zaidi, kupata tafsiri za ziada, au kujiunga na jitihada hizi kupitia Mtandao na Mshikamano wa Afya ya Akili ya Wahamiaji (IMHSN), tafadhali tembelea tovuti yetu